

# Ilala wajipanga kutekeleza mradi machinjio ya kisasa

□ NA CHRISTOPHER LISSA

**SIKU** chache baada ya Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, Dk. Ashatu Kijiji, kutangaza kurejeshwa Hazina sh.bilioni tatu, zilizotolewa kwa Halmshauri ya Manispaa ya Ilala, kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Kiwalani, halmashauri hiyo imesema ujenzi utafanyika kama ilivypangwa.

Fedha hizo sh.bilioni tatu, ni sehemu ya zaidi ya sh.bilioni nane zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo, ambapo Hazina iliingiza kwenye akaunti ya Manispaa ya Ilala sh.bilioni tatu kwa ajili ya kuanza mradi.

Hata hivyo, wiki iliyopita, Naibu Waziri Dk. Ashatu, akiwa katika ziara yake ya kukagua miradi ya kimkakati, alisikitishwa na hatua ya manispaa hiyo kushindwa kuanza mradi huo, hivyo kuagiza sh.bilioni tatu zilizokuwa zimeingizwa katika akaunti ya manispaa, kurejeshwa katika akaunti ya Hazina.

Akizungumza na Uhuru, Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala, Omari

Kumbilamoto, alisema mradi huo utajengwa kama ilivypangwa.

"Baada ya ziara ya Naibu Waziri (Ashatu), tulikaa katika kikao cha majumuisho. Kikao kilihudhuriwa pia

**Baada ya ziara ya  
Naibu Waziri (Ashatu),  
tulikaa katika kikao  
cha majumuisho. Kikao  
kilihudhuriwa pia na  
Mkuu wa Wilaya ya  
Ilala Sophia Mjema na  
watendaji wa halmshauri.  
Waziri aliridhia mradi  
uendelee lakini fedha  
irudi katika akaunti ya  
Hazina,"**


na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Sophia Mjema na watendaji wa halmshauri. Waziri aliridhia mradi uendelee lakini fedha irudi katika akaunti ya Hazina," alisema Kuambilamoto.

Naibu Meya huyo alisema ingawa fedha zitarudi Hazina lakini ujenzi utafanyika na mkandarasi atakuwa akilipwa kupitia Hazina.

"Jiwe la msingi la mradi tutaweka mapema mwezi uja na utaratibu wa ujenzi unaendelea kama kawaida," alisema Kumbilamoto ambaye ni Diwani wa Kata ya Vingunguti (CCM).

Alisema mradi huo ni utekelezaji wa Ilala ya CCM na kwamba ultolewa na Rais Dk. John Magufuli ikiwa ni moja ya miradi mikubwa iliyolenga kukusanya mapato, kuongeza ajira na kuboresha nyama ya Tanzania.

"Niwahakikishie wananchi wa Ilala kwamba serikali yetu ni sikivu na mradi huo utatekelezwa kwa kiwango cha ubora uleule, alisema.



Jumuia ya Wazazi  
kuadhimisha  
wiki ya wazazi  
mwezi ujao

□ NA SIMON NYALOBI

**JUMUIA** ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi(CCM), Mkoa wa Dar es Salaam, inatarajia kufanya maadhimisho ya wiki ya Wazazi mwishoni Machi, mwaka huu.

Akizungumza na Uhuru mwishoni mwa wiki iliyopita, Katibu wa Wazazi, Mkoa wa Dar es Salaam, Geofrey Kavenga, alisema watafanya maadhimisho hayo mwishoni mwa Machi, ili kutoa fursa kwa viongozi wa mkoa huo kuhudhuria maadhimisho ya kitaifa.

Kwa mujibu wa Kavenga, maadhimisho ya wiki ya wazazi yanafanyika Aprili mosi hadi 6, mwaka huu na kwamba wameamua kufanya mapema ili kutoa nafasi kwa viongozi wa mkoa kwenda katika maadhimisho ya kitaifa.

"Tumeona tukjanza kama kalenda inavyosema viongozi wetu wanaweza kuhudhuria katika maadhimisho ya kitaifa, ambayo wanapaswa kuhudhuria ifikapo kilele chake Aprili 6, mwaka huu.

Akizungumzia makongamano